

## **JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



## **WIZARA YA AFYA**

### **HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA ARUSHA – MOUNT MERU**

#### **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MKATABA – MAAFISA TEHAMA**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha – Mt. Meru anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa zinazohitajika na wenye nia ya kufanya kazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha –Mt. Meru kuwasilisha maombi yao.

#### **1. AFISA TEHAMA DARAJA LA II - MWENYE SHAHADA YA UZAMILI (NAFASI 01)**

##### **SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Mhitimu wa Shahada ya uzamili ya Kompyuta katika fani ya Sayansi ya Kompyuta, Uhandisi wa Kompyuta na Teknolojia ya Habari(Information Technology) au mafunzo mengine yanayohusiana na fani hii.
- ii. Awe raia wa Tanzania.
- iii. Awe na umri usiozidi miaka 45.
- iv. Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea.
- v. Asiwe Mwajiriwa wa serikali au mashirika mengine ambaye mshahara wake unalipwa na serikali na Asiwe amewahi kuajiriwa serikalini.

#### **KAZI NA MAJUKUMU YA AFISA TEHAMA DARAJA LA II- MWENYE SHAHADA YA UZAMILI**

- i. Kuweka kumbukumbu na taratibu za kisasa za mifumo pamoja mbinu za kufanya kazi.

- ii. Kuanzisha na kusimamia chati za mtiririko wa mifumo ya nyendo za taarifa na udhibiti.
- iii. Kuandika program za Kompyuta (Implement software systems) Write and document code.
- iv. Kufanya majoribio ya sehemu timilifu za program za Kompyuta (Perform unit systems - module testing).
- v. Kufanya majoribio ya usanifu wa mifumo ya TEHAMA (Perform testing of system configurations).
- vi. Kutengeneza na kufanya majiribio ya program za Kompyuta kulingana na mahitaji ya watumiaji (Conducting user acceptance test).
- vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mwajiri wake wa kazi zinazoendana na sifa na fani yake.
- viii. Kufanya, pia kusimamia kazi za Afisa Tehama daraja la II mwenye shahada zilizoainishwa kwenye tangazo hili.

## **2. AFISA TEHAMA DARAJA LA II– (NAFASI 04)**

### **SIFA ZA MWOMBAJI**

- i. Mhitimu wa Shahada ya Kompyuta katika fani zifuatazo; Sayansi ya Kompyuta, uhandisi wa kompyuta na Teknolojia ya Habari(Information Technology).
- ii. Awe raia wa Tanzania.
- iii. Awe na umri usiozidi miaka 45.
- iv. Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea.
- v. Asiwe Mwajiriwa wa serikali au mashirika mengine ambaye mshahara wake unalipwa na serikali na Asiwe amewahi kuajiriwa serikalini.

### **KAZI NA MAJUKUMU YA AFISA TEHAMA DARAJA LA II**

- i. Uwekaji wa miundombinu mipya ya mifumo, upatikanaji wa teknolojia na ufumbuzi wa programu za uboreshaji ili kukabiliana na mahitaji ya sasa ya kimfumo
- ii. Kufanya kazi za mifumo zinazohitajika na mwajiri kwa viwango vitakavyohitajika.
- iii. Kubuni mbinu za kiufundi zitakazotatua changamoto za kimfumo iliyopo. Mfano: - kubuni mifumo mipya ya kurekodi taarifa za wateja kwa nyakati tofauti tofauti zitakapohitajika.
- iv. Kutoa mahitaji ya kiufundi ya miundombinu ya mifumo ya kutolea huduma za Afya kwa maeneo yote yanayotoa huduma hospitalini.

- v. Kuboresha taratibu za kiufundi za mifumo na kuhakikisha mifumo inafanya kazi ipasavyo.
- vi. Kudhibiti na kudumisha mahitaji ya miundombinu ya ndani ikijumuisha computers, servers, routers, printers, phones, LAN na WAN.
- vii. Kufuatalia na kutatua hitilafu za kimtandao kwenye vifaa vya kusambaza mtandao na vile vya kutolea huduma.
- viii. Kufanya kazi nyingine za ubunifu zitakazorahisisha utendaji kazi kupitia mifumo kadri ya mahitaji ya mwajiri.
- ix. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mwajiri wake wa kazi zinazoendana na sifa na fani yake.

**MAOMBI YOTE YAAMBATISHWE NA NYARAKA ZIFUATAZO:**

- i. Nakala ya cheti cha kidato cha nne /sita.
  - ii. Nakala za Vyeti vya Taaluma.
  - iii. Maelezo binafsi (CV), yakionyesha umri, anuani kamili na namba ya simu ya kiganjani, pamoja na anuani /namba ya simu za wadhamini wasiopungua wawili.
  - iv. Picha aina ya Pasipoti 2.
  - v. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
  - vi. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 28/11/2022.
- Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya posta au moja kwa moja:-

**MGANGA MFAWIDHI,**

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA WA ARUSHA – MT.MERU,**

**S.L.P 3092,**

**ARUSHA.**

**Imetolewa na Ofisi ya Habari na Uhusiano  
Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha – Mt.Meru  
17 Novemba, 2022**